JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

S.L.P. 38 KYAKA - KAGERA

Kumb. KGR/MSY/ S.2/3/VOL.III/59 04/10/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Missenyi anatangaza nafasi ishirini na nane (28) za wakusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya na nafasi nne (4) za Madereva. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi kama zilivyoainishwa hapa chini:-

I. WAOMBAJI WA NAFASI YA KUKUSANYA MAPATO (NAFASI 28)

1. SIFA ZA MWOMBAJI.

i. Awe na Umri wa kuanzia miaka 18-45
ii. Awe na Elimu ya kidato cha nne
iii. Awe raia wa Tanzania
iv. Awe na uwezo wa kutumia mashine ya kukusanyia mapato – akifundishwa.
v. Awe na Wadhamini 2 wenye mali isiyohamishika
vi. Awe mwaminifu, na mchapa kazi
vii. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwenye kituo chochote atakachopangiwa kufanya kazi.

2. MAJUKUMU YA KAZI :

i. Kukusanya mapato ya Halmashuari katika kituo chochote atakachopangiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.
ii. Kutunza vifaa atakavyokabidhiwa katika utekelezaji wa majukumu yake.
iii. Kuweka fedha zote atakazokusanya kwa muda kulingana na taratibu za fedha.
iv. Kuripoti kwa mwajiri juu ya uharibifu wowote wa vifaa atakavyokabidhiwa pale tu unapotokea.
v. Kuhakikisha risiti ya kieletroniki yenye usahihi na uhalali wa malipo inatolewa kwa mlipa ushuru / kodi.

vi. Kutoa taarifa ya haraka ya ukwepaji wa ushuru / kodi kwa mamlaka husika pale ukwepaji unapofanyika au kuonekana unatakakufanyika.

II. WAOMBAJI WA NAFASI YA UDEREVA (NAFASI 4)

1. SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe na Elimu ya kidato cha Nne (Form IV)
ii. Awe na Leseni Daraja la E au C ya Uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (!) bila kusababisha ajali.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari 'Basic Driving Course" yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
iv. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

2. MAJUKUMU YA KAZI:-

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
vi. Kufanya usafi wa gari.
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

III. MASHARTI YA JUMLA

i. Mwombaji aambatishe, maelezo binafsi yanayojitosheleza **(detailed C.V)** yenye anwani na namba za simu za wadhamini (referees) wawili wa karibu.
ii. Maombi yote yaambatane na cheti cha kuzaliwa, taaluma, maelezo na nakala za vyeti vya kidato cha nne na vyeti vingine vya kitaaluma.
iii. Maombi yote yapitishwe kwa Mwenyekiti wa Kijiji au Mtendaji wa Kijiji vilevile wadhamini wa mwombaji wathibitishwe na ofisi ya mtendaji wa Kijiji husika.
iv. Barua zote zipitie posta na hakuna barua itakayopokelewa bila kupita posta na maombi ambayo hayatapita posta hayatashughulikiwa.
v. Mwombaji aambatanishe picha mbili za paspoti size za rangi.
vi. Barua iandikwe kwa mkono.
vii. Mwombaji aambatanishe cheti cha NIDA au namba ya NIDA.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 14 Oktoba, 2022 siku ya Ijumaa saa tisa na dakika 30

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi,
S.L.P 38,
KYAKA – MISSENYI.

Wazili K. Kombo
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

NB: *Wakusanya Ushuru waliopo kazini hadi sasa wanatakiwa kuomba upya ajira hii kwa kufuata utaratibu ulioonyeshwa hapo juu.*